

MAHOJIANO NA BEN R. MTOBWA

MIKHAIL D. GROMOV

Mahojiano haya yamefanyika tarehe 11 Januari 2008, mjini Mainz, Ujerumani, wakati wa Kongamano la Tisa la Janheinz Jahn “Beyond ‘murder by magic’: investigating African crime fiction” lililofanyika Chuo Kikuu cha Mainz.

MG: Kwanza kwa niaba yangu na ya watu wote walioandaa kongamano la tisa la Janheinz Jahn ningetaka kukushukuru, bwana Ben Mtobwa, kwa kukubali kufanya haya mahojiano juu ya uandishi wa riwaya za upelelezi Tanzania kwa jumla na, bila ya mashaka, juu ya uandishi wako. Swali langu la kwanza ni: kwa mujibu wa hali ya mambo, Tanzania imeshazaa, tuseme, waandishi wengi walioandika na wanaoendelea kuandika riwaya za upelelezi. Kwa upande mwingine, huko Kenya – bila ya mashaka ni nchi itumiayo Kiswahili na ambayo sasa inajaribu kuhamasisha na kukuza hadhi ya Kiswahili nchini – lakini mpaka sasa palikuwa na jaribio moja tu, palikuwa na mwandishi mmoja tu Mkenya ambaye aliandika riwaya tatu, kama ninavyokumbuka, za upelelezi kwa Kiswahili. Kwa maoni yako sababu mojawapo ingeweza kuwa nini?

BM: Kwa Wakenya kutokuandika mno upelelezi... Mimi nadhani kitu kikubwa ni kwamba wao walikuwa waandishi wa mambo mengi ya kiutawala, uchumi wa nchi, kama akina Ngugi, akina nani wameandika juu ya utawala. Kwa hivyo nadhani wengi wao mfumo wao wa uandishi ulielekea kwenye upande mmoja. Kwetu wakati ule, haswa wakati wa ujamaa, ukiandika mno juu ya mambo ya utawala, labda *kuchallenge* serikali au chama tawala, ulikuwa unapata taabu. Kwa hivyo nadhani waandishi wa kwetu Tanzania walifikiria kuhamia kwenye upande wa kuandika vitabu ambavyo havitaunganishwa na *government* ya utawala uliokuwepo kwa wakati huo. Kwa mfano, Kenya yule Ngugi alikaa ndani muda mrefu kwa ajili ya kuandika vile vitabu ambavyo vilikuwa vina kuwaudhia. Nadhani ilitupa hofu kidogo watu wa Tanzania ambaa waliishia kwa kuandika vitabu vingi visivyohusika na utawala.

MG: Wakati ule ule Wakenya wameshaandika riwaya nyingi za upelelezi kwa Kiingereza, lakini kuna riwaya tatu tu kwa Kiswahili – kwa nini?

BM: Hivyo nadhani ni kwa ajili ya *market*, soko lililopo kule Kenya kwa *English* ni kubwa kuliko kwetu. Kwetu ukijaribu kuandika kwa Kiingereza inabidi utafute *publisher* wa nje na *market* ya nje kuliko ya pale ndani. Nadhani lugha ya kwetu pale ya Kiswahili ni kweli *around* na kila kitu.

MG: Sasa swali moja kuhusu hali iliyopo juu ya riwaya ya upelelezi kwenye fasihi ya Tanzania. Kama tunavyokumbuka wote, mnamo miaka sabini na themanini na hata nafikiri

MIKHAIL D. GROMOV

tisini palikuwa na waandishi wengi walioandika riwaya za upelelezi na bila ya mashaka idadi ya riwaya hizo ilikuwa ni kubwa sana. Yaelekeea kuwa siku hizi, mwanzoni kabisa ya karne ya ishirini na moja, idadi ya riwaya za upelelezi zilizoandikwa na waandishi wa Tanzania imekwenda chini sana. Kuna sababu fulani kwa hiyo?

BM: Sababu nadhani kuna nyingi kidogo. Nadhani mojawapo inayofanya watu washindwe kuandika ni wachapishaji washindwe kupokea vitabu vipyta. Na wachapishaji wanaogopa kupokea vitabu vipyta kutokana na shida ya biashara. Biashara ya vitabu inaendelea kupungua, watu wengi hawana hela, na nadhani ni hali ya uchumi vile vile. Katika miaka hii kumi na ngapi uchumi wa kwetu umeshuka kuliko ulivyokuwa. Namba ya mbili nafikiri ni vijio vya vitu kama *video* na nini... maanake leo mtu anaangalia *video* ya labda Rambo anavyofanya vitu vya ajabu kule Marekani. Anakuta ni afadhali kuangalia kwa masaa kuliko kununua vitabu vya Joram Kiango au labda vitabu kwa wadogo kama *Sokoni Kariakoo*. Kwa hivyo nadhani yale mambo yameshaingia. Ni ya pili, na ya tatu ambayo ni kubwa kwa wote ni ya moyo ambaa umeshuka, umepungua mno. Watu wengi wamepunguliwa na tabia ya kusoma.

MG: Na unafikiri ile tabia ya kusoma imepungua kwa sababu ya nini? Kwa sababu ya kuingilia kwa mambo ya runinga ama...?

BM: Naam, nafikiri runinga imeshaingia, lakini ni pia kwamba vitabu vipyta hakuna, vingi utakuta ni vile vile, labda kikitoka kimoja mnamo miaka miwili. Kwa hivyo kuna wale ambaa wanavipenda vitabu wamevunjika moyo, na hawa wengine ambaa ni jamii mpya hawaoni vitabu, ndiyo nadhani ni chanzo. Lakini nadhani vile vile kitu kingine kikubwa ni mfumo wa utawala. Vitabu vya riwaya vya kawaida havinunuliwi hata mara moja na mserikali, hata mara moja, wala hawavihitaji na hawachukulii kama ni vitabu. Kwa hivyo wanapenda vile vitabu vya kufundishia tu, ambavyo viko kwenye kiada, vitabu vya primary, vitabu vya sekondari, vile vipyta ambavyo vinatumika labda shule. Ukitafuta wanataja kwamba wanunuua vitabu fulani, lakini wao hawatoi hela kwa kununuua vitabu vya hadithi au vya riwaya, hata mara moja.

MG: Basi kutokana na hiyo, kwa maoni yako, katika fasihi andishi ya Tanzania ya kisasa riwaya ya upelelezi inachukua bado mahali fulani, na mahali gani?

BM: Mimi nadhani ile kidogo inafanya watu wapende vitabu, maanake mtu hahitaji kufikiri mno kwa kuielewa, halafu anaburudika. Kwa hivyo inachochea kidogo uandishi – kidogo ila tu, kutokana na watu kutokuwa na hela, bei ya vitabu ni kubwa, wanashindwa. Lakini nadhani mchango wake ni mkubwa mno katika jamii kuliko riwaya ya kawaida.

MG: Juu ya mchango wa riwaya ya upelelezi na riwaya ya kawaida – palikuwa na mchunguzi fulani wa fasihi wa Kiitalia, kwa jina la bwana Moretti, ambaye alipozungumzia wakati fulani riwaya zilizoandikwa na Agatha Christie, ye ye alisema kuwa kwa kweli riwaya ya upelelezi haiwezi kumfaa msomaji maishani, riwaya ya upelelezi haimfundishi msomaji mambo ya kufaa juu ya maisha. Ungekubali na maoni haya?

MAHOJIANO NA BEN R. MTOBWA

BM: Mimi nitatofautiana naye, maanake kitu kikubwa kimoja ni kumfanya mtu apende kusoma vitabu, bila kujali ni riwaya ya namna gani. Kwa hiyo ile peke yake ni hatua moja – mtoto apende kitabu hiki baadaye atapenda kitabu cha pili, ni namba moja. Namba mbili inategemea hii riwaya ilikuwaje, lakini katika riwaya nyingi kutoka labda kwetu Afrika Mashariki kuna kitu fulani ambacho kinafundisha watu, ambacho ni ukweli. Kwa mfano, kuna kuandika juu ya hujuma ya uchumi ya nchi. Hata kama baadaye utakuta yule mtu hamwamini kuwa yule mhusika huwa hafi, lakini kwenye novel labda mtu atainunua [kwa sababu ya] *detective work*, au [kwa sababu ya] yule *character*. Kwa hivyo inafundisha nadhani. Na namba *two* ni kwamba kama tulivyoongea pale utawala watu wanaogopa kuandika *direct* vitabu wanavyoshambulia utawala, lakini wanapitisha kwenye riwaya hiyo mambo yote waliyotaka kuandika mle, na yanakwenda, na watu wameyaelewa. Na huo nadhani ni mchango mkubwa kuliko ilivyoliliwa na huyo bwana aliyeitwa Moretti.

MG: Mahali pakubwa kwenye uandishi wako panachukuliwa na riwaya zako juu ya Joram Kiango, basi maswali machache juu ya riwaya hizo. Kwanza – ulipoanza kuandika hizo riwaya, na unapoendelea kuandika hizo riwaya sasa, ulilenga na unaendelea kulenga hadhira gani?

BM: Mimi nadhani nawalenga vijana, maanake vijana ndio wanaopenda vitabu vyta aina ile, na vijana ndio tunaowapa, tunawatia moyo wa kupenda vitabu, kwa hiyo nadhani nalenga vijana. Lakini kuna watu wakubwa wengi vile vile amba wanapenda vile vitabu. Kwa mfano unapoacha kuandika kwa miaka miwili mitatu utakuta anakuuliza “mbona hukuandika bado kitu”. Kwa hivyo nadhani jamii yote hupata faida kwa namna fulani.

MG: Kuhusu jambo lile lile – kwenye makala yangu ambayo nimeitoa kwenye kongamano hilo nilithubutu kufikiri kuwa katika riwaya zako juu ya harakati za Joram Kiango ulikuwa na bado upo na ujumbe mwingine, ujumbe tofauti kuliko ile ploti yenye. Kwa sababu katika riwaya hizo, haswa nafikiri katika riwaya zilizotolewa hivi karibuni, kuna mapicha mengi ya hali halisi ya mambo ya kijamii nchini Tanzania. Na pia kwa maoni yangu haya mapicha hayana uhusiano wa moja kwa moja na ploti na hadithi yenye. Ulikuwa na ujumbe gani, ulitumia huu mtambo wa kimtindo kwa ajili ya nini?

BM: Unajua wakati fulani, wakati namleta Joram kwenye vitabu vyangu, ni wakati tulikuwa na kitu kinaitwa *cold war* – vile vita baridi baina ya Mashariki na Magharibi. Kwa hivyo wakati ule tulikuwa na mambo mengi ya kuandika juu yao ya kimataifa. Lakini hivi karibuni mambo yamebadilika, shida tunavyoiona haitoki tena nje – inatoka ndani. Watu wetu mle ndani ndio wengi wanakuwa hushirikiana na watu wanaohujumu uchumi wa nchi, wao wenye wahuju mu tulicho nacho, kwa hivyo tunavyoandika kwa vyo vyote hali ya katikati imebadilika; nafikiri hakuna mahala pa kuhangaika, na mambo yaliyo ya hewani – tuandike yale ambayo tunayapokea nyumbani kwetu, bila kubuni ya hayo mengi ambayo tuliyaandikia.

MG: Yaani pamoja na kumburudisha msomaji na hadithi yenye, hadithi ya kumshika tangu mwanzo hadi mwishoni, pia unatarajia kumwelimisha kijamii?

MIKHAIL D. GROMOV

BM: Bila shaka ni hivyo. Unapomwambia vitu ambavyo pengine alikuwa havifahamu vyote na anaviona kijuujuu, unamwekea kwenye riwaya, nadhani anaelimika kwa kutosha.

MG: Kitabu chako cha kwanza kilichochapiswa mnamo miaka themanini kilikuwa ni riwaya *Lazima Ufe Joram*. Kwa nini umeamua kuendelea na njia yako kama mwandishi na riwaya ya upelelezi, si riwaya za kawaida, riwaya za kijamii?

BM: Nafikiri kitu kikubwa ni kile kwamba tayari nina washabiki; ni watu ambao ukikaa kimya wanakupigia kelele, wanataka riwaya nyingine ya Joram, wengine unakuta walikuwa wamepata vitabu vyote na pamoja mpaka namba kumi. Kwa hivyo kuna watu hawakubali kwamba uishie hapa, wanataka uendelee na vitabu vipy.

MG: Lakini juu ya kile kitabu chako cha kwanza – kwa nini umeamua kiwe riwaya ya upelelezi na si riwaya ya aina nyingine?

BM: Wakati ninachapisha kile nilikuwa na riwaya tatu: nilikuwa na ile ya *Zawadi ya Ushindi* tayari, nilikuwa na... nafikiri mbili. Kwa hiyo ile... actually nilipoitao nikiipeleka kwenye vyombo vya habari, na palikuwa na rafiki yangu moja akiwilling kuihakiki. Akaipenda, akaenda kwenye vyombo vya habari, na mwishowe mimi niliona imeshatoka. Lakini nilipokubalika nипанue ndiyo kidogo, ilinipa moyo kwa kuandika riwaya moja ya Joram Kiango.

MG: Pia juu ya tanzu yenyewe ambayo unaitumia – kama siyo riwaya ya upelelezi ya kawaida, lakini zaidi ni riwaya ya kijasusi – na mhusika mwenyewe, Joram Kiango. Ulipoanza kubuni hizo riwaya, ulipoanza kumbuni yule mhusika – umeathiriwa na uandishi fulani kutoka magharibi au ya kimataifa?

BM: Kwa kweli nilivutiwa na waandishi wengi mno, nikiangalia kitabu hiki na kile... vitabu vingi vilinivutia. Na baada ya kunivutia mimi niliona nibuni kitu ambacho kitakuwa kidogo na tofauti na vile, lakini pia upande wa upelelezi. Kwa hivyo hapo nimembuni Joram Kiango. Nadhani hakuna namna ya mwandishi ye yote kuandika kitu kutoka hewani bila ya kuvutiwa na kilicho mwandishi mwingine alichobuni.

MG: Waandishi gani, kwa mfano?

BM: Mm... nadhani majina yamenitoka; ni waandishi ambao waliandika vitabu vya aina ile. Kwa mfano kuna mwandishi mmoja aliyejkuwa aliandika vitabu vilivyoshughulika na jamii ya Uingereza, miaka kumi na kadhaa hivi, ambaye alikuwa kidogo ni tofauti; nadhani nikitatufuta jina nitakumbuka.

MG: Yaani hukuathiriwa na waandishi wo wote maarufu upande wa riwaya za upelelezi – kama James Hadley Chase, kama Raymond Chandler, na wengine?

BM: Nimevisoma vitabu hivi, kila kina vitu vyake, lakini bila ya kunivutia, maanake niliona vingi vilifuata mfumo wa aina moja. Kwa ujumla wao walioniathiri ni wale waandishi wa

MAHOJIANO NA BEN R. MTOBWA

Kiafrika wa namna ya kijamii, kama akina Ngugi, wao waliniathiri kuliko waandishi wa upelelezi.

MG: Yaani ulipoumba yule mhusika mkuu wako Joram Kiango hukufuata mfano wo wote, hukufuata mfumo wo wote ulio tayari?

BM: Nadhani nimefuata, yule kwa kukumbuka kwamba nadhani alinishawishi, ulikuwa ni muda mrefu wakati ule – nafikiri ni miaka ishirini na tano, thelathini na sita, inakuwa vigumu kukumbuka – lakini nadhani vilikuwa ni vitabu vingi wakati ule vilivyonivutia, hata vya watoto, ambavyo vinaonyesha upelelezi – vilinivutia. Nakumbuka kila kitabu ninachokipata nakiangalia na kutatanisha.

MG: Euphrase Kezilahabi mnamo miaka sabini alisema kuwa – kwa Kiingereza – “at best Swahili detective novels published so far look like carbon copies of American crime stories and movies”. Uliathiriwa na filamu fulani fulani juu ya ujasusi ama upelelezi ulipoandika riwaya juu ya Joram Kiango – kama zile filamu za James Bond au nyingine?

BM: Hata kama kwangu film ina faida yake, vilivyonithiria vitakuwa ni vitabu. Lakini kauli ya bwana Kezilahabi nadhani natofautiana naye. Naam, nakumbuka kitabu kimoja, kama *Dar es Salaam Usiku*, – kulikuwa na workshop moja kufanyika pale na kushirikiwa na mtaalam mmoja wa fasihi, yeye alikuwa ni mtu ambaye akiponda tu kile kitabu, kwamba ni uhuni tupu na kina mambo ya kuhujumu amani, lakini walikuwa wakubwa wengine, kwa mfano, Kezilahabi na yule nani... Mulokozi – aliinuka pale alikitetea vibaya mno, na akakiweka kile kitabu katika *group* moja na vitabu vya Kezilahabi, kama hakuna tofauti. Kwani nadhani vilikuwa ni *controversial*, vile vitabu.

MG: Kuhusu uwezekano wa vitabu kupelekeea kwa wasomaji ujumbe wa kijamii – kando ya kuziandika riwaya nyingi za upelelezi umeziandika na ulichapisha riwaya mbili ambazo nafikiri tungeweza kuziita kama riwaya za kijamii, riwaya za kuhakikia hali ya kijamii. Riwaya hizo ni *Pesa Zako Zinanuka* na *Dar es Salaam Usiku*. Umeamua kuziandika kama riwaya zako za pekee za kijamii, kando ya riwaya za upelelezi, kwa sababu gani? Labda hukuona kuwa riwaya za upelelezi zinaweza kuapelekeea wasomaji ujumbe wa kijamii wa kutosha?

BM: Kwa kweli ilikuwa ya tatu ambayo hukuitaja, inaitwa *Zawadi ya Ushindi*, ambayo nafikiri ilikuwa kitabu changu cha pili au cha tatu *kuattempt* kuandika, lakini kikuja kutoka baada ya miaka kumi, kwani nilikuwa na mashaka kama labda itapendwa na nini... Kwa hivyo kwa ujumla nilikuwa nategemea naandika hivyo naangalia watu wanapendelea nini. Na riwaya nyingi kabla ya kuchapisha vitabu wanatoa kwenye vyombo vya habari, magazeti, na kama wanakuta watu wanavutiwa na ile, wanaamua kuchapisha kitabu kwa hivyo. Kwa mfano, Joram namba moja – kilitoka kwenye gazeti la kikatoliki lilioitwa *Kiongozi* kwa muda mrefu, na wao nadhani hata walilinunua kwa ajili ya ile hadithi. Hivyo vitabu vingi vya kijamii vilivyojaribu kutawanyika, na vinapendwa, kwa mfano kama hiyo *Zawadi ya Ushindi*,

MIKHAIL D. GROMOV

vinatumika mashulen, wameshaitumia kwa muda wa miaka kumi, ila wakati huo kulikuwa na hujuma.

MG: Kwa ukamilifu zaidi, swali langu lilikuwa ni: kwa sababu gani siku moja umeamua kuziandika hizo riwaya za kijamii, riwaya zinazohakikia hali ya kijamii, bila ya kuzitilia yale mambo ya upeletezi?

BM: Mimi nadhani kitu ni kwamba kuna kitu ambacho unashindwa kukiweka, kwa mfano, kama ni vitabu ambavyo unaviweka Joram Kiango. Kuna watu wengi wamekuwa walilalamika, kwa mfano, marehemu Chachage, anapenda kwa hali ya mbele *Nyuma ya Mapazia*, lakini akifika mahali pa kumweka Joram Kiango ndani, aliacha kile kitabu. Kwa hivyo kuna watu amba wanatafuta, au wanapenda kuwafikiria, amba hawataki mambo ya upeletezi, ndio wanaotaka mambo ya kijamii moja kwa moja. Kwa hivyo hao nadhani ninawafikiria wakati naandika riwaya za kijamii. Ninacho kitabu kimoja kikubwa, kinaitwa *Kiguu na Njia*, ni *character* aliyetembea karibu kila mkoa, na anaangalia uchumi wa nchi, history, geography, na kila kitu. Ni kikubwa na kinavutia, lakini unafikiria mara nyingine swali la kuchapa, na unafikiri kuwa labda kwa hela hii utachapa vitabu vingine vitatu, ingawa hiki ni cha kijamii ambacho ni bora kuliko vitabu vyote vyangu vya kijamii vya wakati huu.

MG: Swali jingine na lisiloepukika, kwa sababu pameshakuwa na mazungumzo mengi juu ya hiyo. Katika riwaya yako ya *Dar es Salaam Usiku* kuna sehemu fulani zinazochorea mapenzi ya kimwili baina ya mwanamume na mwanamke. Profesa Bertoncini ameshaiita Dar es Salaam Usiku kwa Kiingereza “the first erotic novel in Swahili fiction”. Umeweka picha hizo za mapenzi ya kimwili katika riwaya hii kwa ajili ya nini?

BM: Nadhani nilitaka kuandika ukweli wa maisha badala ya kuficha. Utakuta mpaka leo katika miji yetu ya Afrika kuna watu wengi – akina mama, watoto wadogo – ambao biashara yao ni mwili, wanategemea mwili kwa kupata chakula chao, kuna maradhi kama ukimwi, lakini hawaogopi. Kwa hiyo niliamua katika kitabu kile niweke mambo kidogo kila mtu ayaone kama yalivyo, bila ya kuficha kwa mbali; naficha, lakini kwa kiwango fulani, na nadhani naweza kukubalika na hiyo.

MG: Sasa ni swali la kawaida linaloulizwa mwishoni mwa kila mahojiano: mipango yako kwa nyakati zijazo?

BM: Nimejaribu kuingia kwenye mambo ya filam kidogo, kwa ajili ya kwamba nia yangu ni *kuwatouch* watu wote ambao *hawakutouched*, kwa hivyo kuna vitabu ambavyo ninajaribu kuviweka kwenye filam. Bado tunashindwa kidogo na *capital*, lakini nadhani kama nitatulia kidogo ndiyo njia ya kufanya kila mpango utimizwe. Lakini vile vile nitaendelea kuandika mpaka mwisho wa uhai wangu.

MG: Je, tutapata vitabu vipyta vya Joram Kiango?

BM: Nadhani kabla ya mwisho wa mwaka huu nitatoa kitabu kipyta cha Joram Kiango. Sijapata jina, lakini nadhani kitakuwepo.